



Kukaa kushikamana



Kukaa na uhusiano na jumuiya yako inaweza kukusaidia kukaa nchini Australia.



Kujihisi kushikamana na marafiki pamoja na jamii yako walio nchi za ng'ambo ni muhimu.

Klabu ya jamii na kijamii



Kuna huduma nchini Australia ambazo zinaweza kusaidia wahamiaji.

Wewe unaweza kuungana na watu katika eneo lako kwa kujiunga na makundi ya jamii au jamaa, ikiwa ni pamoja na:



- mashirika ya jamaa



- vilabu vya michezo



- vikundi vya kijamii



Wewe unaweza kuwa na uzoefu mpya.




Wewe unaweza kuendelea kushiriki katika maslahi pamoja na shughuli ambazo tayari wewe unafurahia.

Maktaba



Maktaba ya umma yana mambo ya kusoma kwa lugha nyingi.



Wewe unaweza:

- kuvisoma maktabani



- vikopesha na kuchukua nyumbani



Maktaba mengi pia yana:

- kompyuta unazoweza kutumia




- uwezo bure wa kutumia mtandaoni

Televisheni pamoja na redio



Huduma Maalum wa Utangazaji (Special Broadcasting Service - SBS) hutoa habari katika lugha nyingi tofauti.



Wewe unaweza kuangalia SBS kwenye televisheni.



Wewe unaweza kusikiza SBS kwenye redio.

Simu



Unaweza kupiga simu kwa kutumia:

- simu ya nyumbani
- simu ya mkono

Simu ya nyumbani




Mpangilio ni simu inayounganishwa na nyumba yako.



Kuna makampuni mengi ambayo yanaweza kuunganisha simu na nyumba lako.




Kunao uwezekano kuwa lazima ulipie ada ya uunganisho.



Wewe utapata bili kila mwezi kwa simu unazofanya kutumia simu hiyo.

Simu za mkononi



Simu za mkononi zinaweza kuwa kitu muhimu kuwa nawe lakini zinaweza kuwa na gharama nyingi kutumia.




Simu yako ya mkononi inaweza kuwa:

- kulipwa kabla ya matumizi
- kwenye mpango wa simu uliolipwa kila mara



Simu za kulipwa kabla ni nzuri kama unataka kupunguza kiasi gani unachotumia – huwezi kutumia zaidi kuliko unayoweza kujimudu.



Wewe unalipa kabla ya kutumia simu.

Hii inaitwa mkopo.




Ikiwa unatumia mkopo wako wote huwezi kutumia simu mpaka unapoongeza zaidi.



Katika mpango unastahili mkataba.



Wewe utalipa kiasi sawa kila mwezi.



Kutakuwa na kiasi cha simu ambacho unaweza kufanya.



Ikiwa wewe unafanya simu zaidi kuliko mpango wako inakuwezesha kulipa ziada.



Simu za eneo la mtaa wako hazina gharama kubwa sana.



Inaweza kukugharimu wewe pesa nyingi kupiga simu kwa maeneo yaliyo:

- katika Australia lakini mbali sana
- ng'ambo



Wewe unaweza kununua kadi za simu ambazo unaweza kutumia kutumia simu za nje ambazo zina gharama kidogo.

Barua



Wewe unaweza kuzituma barua pamoja na vifurushi kwenye anwani yoyote ile katika:

- Australia
- mahali pengi ng'ambo



Wewe unaweza kununua stampu kutoka kwa ofisi za posta.




Inakugharimu zaidi kutuma vitu ng'ambo.

Tuvuti



Mtandao ni njia inayosaidia kukaa kushikamana.


Ili kutumia mtandao nyumbani wewe unahitaji:



- kompyuta



- uhusiano wa mtandao




Wewe unaweza kupata uhusiano wa mtandao kupitia Mtoaji wa Huduma ya Mtandao (Internet Service Provider - ISP).




Kunazo ISP nyingi. Unapaswa kuzungumza na ISP chache kabla ya kuchagua:

- ISP
- mpango wa ISP



ISPs zina mipango tofauti ya kuchagua.

Mipango hukupa data ya kutumia ambayo unalipa kila mwezi.



Wewe unaweza pia kutumia simu za mkononi na vibao kufikia mtandao.



Simu za mkononi pamoja na vibao ni kompyuta ndogo zilizo na skrini za kugusa.



Zinaweza kuwa rahisi kutumia lakini inaweza kuwa na gharama kidogo zaidi.



Wewe unaweza kutumia kompyuta kwenye maktaba yako ya eneo kwa bure ikiwa:

- huna kompyuta
- huna uhusiano wa mtandao



Mfanyakazi wa maktaba anaweza kukusaidia ikiwa hujawahi kutumia kompyuta au husijihisi kuwa mtu mjasiri.

Ukurasa huu umewachwa tupu makusudi



Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji
la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya
Huduma za Jamii nchini Australia

